JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# TAARIFA KWA UMMA

## WITO WA KUCHAGUA MIRADI YA TEHAMA KUTOKA TANZANIA ILIYOAINISHWA KUSHINDANA KWENYE TUZO ZA WSIS 2025

Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU) kwa kushirikiana na Mkutano wa Dunia wa Jumuiya ya Habari (WSIS) na waratibu wake wa sherehe ya tuzo za WSIS 2025 kwenye tukio la mkutano wa kilele wa WSIS+20. WSIS ni mfululizo wa mikutano inayofadhiliwa na Umoja wa Mataifa, ikiwa na lengo la kujadiliana kuhusu fursa na changamoto zinazoletwa na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika zama hizi za taarifa.

Kufuatia Taarifa kwa Umma iliyotolewa na TCRA tarehe 29 Oktoba 2024. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kama mratibu inawashukuru wadau wote waliowasilisha miradi yao, na tunayo furaha kuwajulisha Umma kwa ujumla na wadau wa WSIS kuwa miradi kumi na nne (14) kutoka Tanzania imeainishwa kwaajili ya kuchaguliwa. TCRA inahimiza Umma kwa ujumla, zikiwemo taasisi za Serikali, sekta binafsi, taasisi za kimataifa na kikanda, asasi za kiraia na wanataaluma kuchagua miradi hii kabla au ifikapo 30 Aprili 2025 ili kuipa nafasi miradi ya Tanzania kushinda tuzo hizi.

Orodha ya miradi iliyochaguliwa kutoka Tanzania kwa Tuzo za WSIS 2025

| S/N | Na. Lengo | Lengo | Jina la Mradi | Taasisi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Lengo Na. 1 la WSIS (AL C1), Category 1 | Nafasi ya Serikali na wadau mbalimbali katika kukuza TEHAMA kwa maendeleo.<br><br>(*The role of governments and all stakeholders in the promotion of ICTs for development*) | Uboreshaji Mipango, Uandaaji wa Bajeti na Utoaji wa Taarifa katika Serikali za Mitaa<br><br>**(*Enhancing Planning, Budgeting and Reporting in Local Government Authorities*)** | TAMISEMI |
| 2. | Lengo Na. 2 la WSIS (AL C2), Category 2 | Miundombinu ya TEHAMA.<br><br>(*Information and communication infrastructure)* | Mradi wa Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano vijijini, Zanzibar<br><br>**(*Rural Telecommunication Project in Zanzibar*)** | Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) |
| 3. | Lengo Na. 3 la WSIS (AL C1), Category 3 | Upatikanaji wa taarifa na maarifa<br><br>*(Access to Information and Knowledge)* | **Mtandao Point** | Mtandao Point |
| 4. | Lengo Na. 5 la WSIS (AL C5), Category 5 | Kuimarisha imani na usalama katika kutumia TEHAMA<br><br>*(Building confidence and security in use of ICT)* | **Apps and Girls** | Apps and Girls |
| 5. | Lengo Na. 5 la WSIS (AL C5), Category 5 | Kuimarisha imani na usalama katika kutumia TEHAMA<br><br>*(Building confidence and security in use of ICT)* | Shindano la ***CyberChampions*** | Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) |

| S/N | Na. Lengo | Lengo | Jina la Mradi | Taasisi |
|---|---|---|---|---|
| 6. | Lengo Na.7 WSIS (AL C7),Category 7 | Serikali Mtandao *(E- Government )* | *Maradi wa* ***AI Powered eMrejesho V2*** | Mamlaka ya Serikali Mtandao – eGA |
| 7. | Lengo Na.7 WSIS (AL C7), Category 7 | Biashara Mtandao (*E-business*) | Mfumo wa Anuani za makazi<br><br>***(National Physical Addressing System (NAPA))*** | Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (MCIT) |
| 8. | Lengo Na.7 WSIS (AL C7), Category 10 | Afya Mtandao (*E-Health)* | Dira Mpya ya Huduma za Afya Zanzibar: Umuhimu wa Utambulisho Maalum wa Kidijitali katika Kuleta Mageuzi<br><br>*(**A New Era in Zanzibar's Healthcare: The Game-Changing Role of Digital Unique Ids**)* | PHARMACCESS |
| 9. | Lengo Na.7 WSIS (AL C7), Category 13 | Kilimo mtandao *(E-agriculture)* | Kuwezesha Kilimo Kinachostahimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia AI na IoT<br><br>**(*AgriSense AS-CRF (AgriSence-Climate-Resillient Farming) with AI and IOT)*** | Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) |
| 10. | Lengo Na.7 WSIS (AL C7), Category 14 | Sayansi ya Mtandao (*E-Science*) | STEM kwa wote **(*STEM 4 All*)** | Chuo Kikuu cha MT. Joseph |
| 11. | Lengo Na.8 WSIS (AL C8), Category 15 | Tofauti za Kitamaduni na Utambulisho, Tofauti za Lugha na Maudhui ya Ndani<br><br>(*Cultural diversity and identity, linguistic diversity and local content*) | Mfumo unaotoa miongozo ya ajira kwa vijana kwa kutumia Akili Unde<br><br>*(**Career Guider AI – AI Powered Career Guidance for Youth Empowerment**)* | Career na Mimi (CNM) |
| 12. | Lengo Na.8 WSIS (AL C8), Category 15 | Tofauti za Kitamaduni na Utambulisho, Tofauti za Lugha na Maudhui ya Ndani<br><br>(*Cultural diversity and identity, linguistic diversity and local content*) | Mradi wa TEHAMA kwa wenye Uziwi ***(ICT for the deaf*)** | Chuo kikuu Huria Tanzania - Kituo cha Ubunifu |
| 13. | Lengo Na.9 WSIS (AL C9), Category 16 | Vyombo vya Habari *(Media)* | Mradi wa **Mwajuma Simama** | Our Voice Againist Harassment |
| 14. | Lengo Na.11 WSIS (AL C11), Category 18 | Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa<br><br>*(International and Regional cooperation)* | Utibuji wa Biomasi kwa Nguvu ya Jua kwa ajili ya Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Mchanganyiko wa Kaboni katika Mfumo Mseto wa Nishati Jadidifu ***(Solar Treatment of Biomass for Power generating using carbon slurries in hybrid renewable energy system)*** | Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) |

**Utaratibu wa Kuchagua Mradi**

1. Ili kuchagua mradi tumia kiunganishi hiki **https://www.itu.int/net4/wsis/stocktaking/Prizes/Prizes/** kujisajili kwenye Jukwaa la WSIS chini ya Tuzo za WSIS PRIZES 2025;
2. Baada ya kujisajili kwa kutumia google account, ingia kwenye mfumo sehemu ya kuchagua imeandikwa “Vote”, utaletewa orodha ya miradi kulingana na lengo (category) kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali la miradi kumi na minne(14) iliyoainishwa kutoka Tanzania;
3. Chagua jina la lengo (category) kisha chagua miradi husika kwa kubofya "Vote for this Project" upande wa kulia wa mradi husika.

**Tafadhali Kumbuka masharti yafuatayo**

1. Siku ya mwisho ya kuchagua ni **tarehe 30 Aprili 2025**, baada ya hapo washindi (90) wa Tuzo za WSIS 2025 watatangazwa na kutambuliwa katika Hatua ya Uteuzi.
2. Kila mwanachama anaweza kuchagua mradi mmoja tu katika kila lengo.
3. Taasisi haziruhusiwi kuchagua mradi wao wenyewe.

Ukomo wa kuchagua ni **tarehe 30 Aprili 2025**.

Imetolewa Tarehe **17 Aprili, 2025.**

Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Thu Apr 17 18:51:05 EAT 2025

CREATING A LEVEL PLAYING FIELD

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
**Simu:** +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 **Nukushi:** +255 22 2412009-10
**Barua pepe:** barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, **Tovuti:** www.tcra.go.tz